**SURA YA 291**

# SHERIA YA HUDUMA ZA JAMII

**SHERIA KUU**

## MPANGILIO WA VIFUNGU

## SEHEMU YA I

## VIFUNGU VYA AWALI


*Kifungu* *Jina*

1. Jina fupi na mwanzo wa kutumika kwake.
2. Tafsiri.


## SEHEMU YA II
## AMRI ZA HUDUMA ZA JAMII


3. Amri za huduma za jamii
4. Wajibu wa mhalifu chini ya amri za huduma kwa jamii
5. Uvunjifu wa amri za huduma kwa jamii
**6.** Mapitio na mabadiliko ya amri za huduma kwa jamii


## SEHEMU YA III
## USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA AMRI ZA HUDUMA KWA JAMII


7. Uanzishwaji wa Kamati ya Kitaifa ya Amri za Huduma kwa Jamii
8. Wajibu wa Kamati ya Kitaifa
9. Kamati ya Utendaji
10. Mratibu wa Kitaifa
11. Amri za Kamati za huduma kwa jamii za Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji
12. Maafisa wa huduma za jamii
13. Maafisa Waangalizi.
14. Kanuni.
15. Uwajibikaji wa Wajumbe wa Kamati ya Amri kwa Huduma za Jamii na Maafisa wengine.
16. Makosa.


---

**MAJEDWALI**

---

## SURA YA 291

## SHERIA YA HUDUMA ZA JAMII

**Sheria kwa ajili ya uanzishwaji na usimamizi wa huduma kwa jamii za wahalifu kwenye baadhi ya mashauri na mambo yanayohusiana na yanayoambatana na hayo.**

[..........................]
Sheria Na. 6 ya 2002

Imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo.

## SEHEMU YA I

## VIFUNGU VYA AWALI

Kichwa cha habari na mwanzo wa kutumika kwake.

**1.** Sheria hii itaitwa Sheria ya Huduma kwa Jamii ya 2002 na itaanza kutumika katika tarehe itakayoteuliwa na Waziri kwenye notisi itakayochapishwa kwenye *Gazeti la kiserikali.*

Tafsiri

**2.** Isipokuwa pale muktadha utakusudia vinginevyo, Sheria hii:-

"Huduma kwa Jamii" maana yake ni mpango unaosimamiwa na Kamati ya Huduma kwa Jamii kwa mujibu wa vifungu vya sheria hii;

"amri ya huduma kwa jamii" maana yake ni amri iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha sheria hii;

"afisa wa huduma kwa jamii" maana yake ni afisa wa huduma kwa jamii katika maana iliyoainishwa chini ya kifungu cha 12 cha sheria hii;

"mahakama" isipokuwa pale muktadha utakusudia vinginevyo, maana yake ni mahakama iliyotoa amri ya huduma kwa jamii na inajumuisha mahakama ambayo ndani ya mamlaka yake mhalifu anaweza kuwa anaishi huku akihudumia kwa mujibu wa amri ya huduma kwa jamii;

"waziri" isipokuwa pale muktadha utakusudia vinginevyo, maana yake ni waziri mwenye dhamana ya wafungwa.

"Kamati ya Kitaifa" maana yake ni Kamati ya Kitaifa ya Amri za Huduma kwa Jamii iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha sheria hii;

"Mratibu wa Kitaifa" maana yake ni Mratibu wa Kitaifa wa Amri za Huduma kwa Jamii aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 10 cha sheria hii;

"mhalifu" maana yake ni mtu aliyetiwa hatiani na kuhukumiwa na

mahakama kwa kosa la uvunjifu wa sheria yeyote ile.

"afisa mwangalizi" maana yake ni afisa aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 13 cha sheria hii ili kusimamia mhalifu dhidi ya utekelezaji wa huduma kwa jamii kwa mujibu wa sheria hii;

## SEHEMU YA II

## AMRI ZA HUDUMA KWA JAMII

Amri za huduma kwa jamii.

**3.** (1) Mtu yeyote atakayekutwa na hatia ya kosa linaloadhibiwa kwa:-

(a) kifungo kisichozidi muda wa miaka mitatu, pamoja na au bila ya mbadala wa faini; au

(b) kifungo kinachozidi muda wa miaka mitatu ingawa mahakama itaamua kiwe kifungo cha miaka mitatu au pungufu, pamoja na au bila ya mbadala wa faini, kama inafaa, mahakama inaweza, kwa mujibu wa sheria hii, kutoa amri ya huduma kwa jamii ikimtaka mhalifu kutoa huduma kwa jamii.

(2) Kwa mujibu wa kifungu hiki:-

(a) "Huduma ya jamii" itahusisha kazi za umma zisizokuwa na malipo ndani ya jamii, kwa faida ya jamii hiyo, kwa muda utakaobainishwa na mahakama ingawa hautazidi muda wa kifungo kama ilivyoainishwa na mahakama kwenye hukumu dhidi ya mhalifu.

(b) "Kazi za umma" zitahusisha ingawa siyo hizi tu:-

(i) ujenzi au ukarabati wa barabara za umma au barabara za kuingilia;

(ii) kazi za uendelezaji misitu;

(iii) utunzaji wa mazingira na kazi za nyongeza;

(iv) miradi ya utunzaji, usimamizi au usambazaji na ugawaji wa maji;

(v) kazi za utunzaji wa mashule ya umma, hospitali na huduma zingine za kijamii kwa umma;

(vi) kazi ya aina yoyote kwenye makazi ya malezi au nyumba za yatima.

(vii) kazi za jumla za usafi na zinazohusiana na hizo;

(viii) kutoa huduma za kitaalamu ndani ya jamii kwa faida ya jamii;

(ix) kazi nyingine za mikono ambazo zitakuwa zikihakikiwa mara kwa mara;

(3) Kwa mazingira yoyote, namna au aina ya kazi ya umma kama ilivyoainishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) hapo juu, zitaamuliwa na mahakama baada ya kushauriana na Kamati ya Amri za Huduma kwa Jamii.

(4) Mahakama inapotathimini utekelezwaji wa amri ya huduma za jamii, inaweza, kabla ya kuitoa, kumuagiza afisa wa huduma kwa jamii kufanya utafiti kulingana na mazingira ya shauri na ya mhalifu na kupeleka majibu ya utafiti huo mahakamani.

(5) Utafiti kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) utafanyika kwa namna inayofaa na taarifa lazima iwe kwenye muundo na uhusishe mambo yote yaliyoelekezwa.

(6) Mahakama haitatoa amri chini ya kifungu hiki dhidi ya mhalifu isipokuwa kama mhalifu yupo na mahakama ikaridhika:-

(a) kuwa mhalifu amekubaliana na amri iliyotolewa;

(b) kuwa upo mpangilio yakinifu wa utekelezaji wa amri; na

(c) baada ya kuzingatia taarifa iliyoandaliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) na kama itakavyolazimu baada ya kumsikiliza afisa huduma kwa jamii, kuwa mhalifu ni mtu anayestahili kutoa huduma za jamii chini ya amri husika.

(7) Mahakama itakapotoa amri kwa mujibu wa kifungu hiki dhidi ya makosa mawili au zaidi yaliyofanywa na mhalifu, mahakama inaweza ikaelekeza kuwa muda wa huduma kwa jamii ulioainishwa utatumikiwa kwa mkupuo ni moja na au nyongeza kama itakavyoainishwa na amri nyingine yoyote.

(8) Mahakama itakayotoa amri kwa huduma za jamii italazimika kutoa nakala za amri hiyo kwa afisa huduma kwa jamii wa eneo husika ambapo mhalifu anaishi au ataishi wakati wa kipindi cha amri na afisa huduma kwa jamii atalazimika kumpa kila mhalifu na afisa mwangalizi nakala ya amri hiyo.

(9) Kabla ya kutoa amri kwa mujibu wa kifungu hiki, mahakama itakayomhukumu mhalifu italazimika kumfafanulia mhalifu kwa lugha anayoielewa:-

(a) madhumuni na athari za amri husika na kwa kipekee wajibu wake chini ya kifungu cha (4);

(b) madhara yaliyoainishwa chini ya kifungu cha (5) kwa kushindwa kutii amri au matakwa yoyote ya kifungu hicho; na

(c) mamlaka ya mahakama chini ya kifungu cha (6) kufanya mapitio ya amri kwa maombi yatakayoletwa na mhalifu au afisa huduma kwa jamii.

(10) Pale mahakama itakapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji thabiti wa amri ya huduma kwa jamii inaweza kumuelekeza mhalifu aingie mkataba pamoja na au bila ya kuwa na wadhamini.

Wajibu wa mhalifu dhidi ya amri za huduma za jamii.

**4.** (1) Mtu anayewajibishwa na amri ya huduma kwa jamii atalazimika:-

(a) kufika kwa afisa mwangalizi aliyebainishwa kwenye amri ili apangiwe kazi; na

(b) atafanya kazi husika kwa kipindi kilichoainishwa kwenye amri katika muda na mahali atakavyoelekezwa na afisa mwangalizi; na

(c) atatoa taarifa kwa afisa mwangalizi mabadiliko yoyote ya anwani yanayoweza kutokea mara kwa mara.

(2) Kwa kadri itakavyowezekana afisa mwangalizi hatakiwi kutoa maelekezo katika kifungu hiki ambayo yatapingana na imani ya kidini ya mhalifu.

Uvunjifu wa amri ya huduma za jamii.

**5.** Ikiwa mhalifu atavunja au atashindwa kutii masharti au matakwa yoyote ya amri ya huduma kwa jamii, mahakama inaweza, kwa maombi ya Afisa huduma za jamii wa eneo husika au afisa mwangalizi kutoa hati wito kwa mhalifu kuja mbele ya mahakama kwa muda utakoainishwa na hati wito au kutoa hati ya kukamatwa kwa mhalifu ili akamatwe na kufikishwa mbele ya mahakama, ikitegemeana na mazingira, na mahakama inaweza, baada ya kumsikiliza mhalifu kufanya yafuatayo:-

(a) kumtahadharisha mhalifu na kumtaka mhalifu kutii amri; au

(b) kufanya marekebisho ya amri kwa namna itakayokidhi mazingira ya shauri; au

(c) ikafuta amri na kupitisha hukumu nyingine yoyote chini ya sheria kama itakavyoona inafaa.

Mapitio na mabadiliko ya amri za huduma kwa jamii.

**6.** (1) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4), mhalifu anaweza kuomba mapitio ya amri ya huduma kwa jamii katika muda wowote baada ya kumtaarifu afisa wa huduma kwa jamii au afisa mwangalizi kwa maandishi mambo ambayo anataka mapitio hayo iyapitie.

(2) Mapitio ya amri yanapokuwayameombwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), afisa huduma kwa jamii au afisa mwangalizi atalazimika kupeleka maombi mahakamani kwenye fomu elekezi itakayoonesha mambo yaliyoainishwa chini ya kifungu hicho na mahakama inaweza kufanya mapitio au mabadiliko ya amri ya huduma kwa jamii.

(3) Bila ya kujali kifungu kidogo cha (2) kwa mazingira maalumu, mhalifu anaweza kupeleka maombi mahakamani bila ya kumtaarifu afisa huduma kwa jamii au afisa mwangalizi na afisa huduma kwa jamii au afisa mwangalizi maombi ya mapitio kwa sababu zozote za msingi.

(4) Ikiwa mapitio au mabadiliko ya amri chini ya kifungu kidogo (1) yatapelekea mabadiliko ya makazi ya mhalifu, mahakama iliyobadilisha amri hiyo itaitaarifu mahakama iliyo na mamlaka kwenye eneo ambalo mhalifu anatarajia kuishi, na itatoa nakala za amri ya huduma kwa jamii itakayowasilishwa kwenye mahakama yenye mamalaka ambayo mhalifu ataishi na kwa afisa huduma kwa jamii wa eneo hilo.

(5) Mapitio ya amri kwa mujibu wa kifungu hiki hayatakuwa ya lazima endapo mhalifu atabadili makazi bila ya kuathiri amri iliyopo au kuwa nje ya mamlaka ya mahakama iliyotoa amri.

## SEHEMU YA III

## USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA AMRI ZA JAMII

Uanzishwaji wa Kamati ya Kitaifa ya Amri za Huduma za Jamii

**7.** (1) Kutakuwa na Kamati ya Kitaifa ya Amri za Huduma kwa Jamii na kwa mujibu wa sheria hii itatambulika kuwa ni “Kamati ya Kitaifa” kwa Tanzania Bara.

(2) Kamati ya Kitaifa itakuwa na:-

(a) Mwenyekiti ambaye atakuwa ni Jaji wa Mahakama Kuu au mtu mwingine yeyote mwenye ujuzi kwenye mambo ya kisheria na mwenye uelewa wa kutosha dhidi ya usimamizi wa haki kwenye makosa ya jinai atakayeteuliwa na Waziri;

(b) Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali au mtu atakayeteuliwa dhidi yake;

(c) Atakayeteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ambayo kwa wakati huo inasimamia mambo yanayohusiana na Mambo ya Ndani;

(d) Atakayeteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ambayo kwa wakati huo inasimamia mambo ya Kazi;

(e) Mkuu wa Majeshi ya Polisi au mtu atakayeteuliwa/chaguliwa;

(f) Kamishna Mkuu wa Magereza au mtu atakayeteuliwa/chaguliwa;

(g) Kamishna wa Ustawi wa Jamii;

(h) Kamishna wa kazi;

(i) Mtu aliyependekezwa na chama cha wanasheria Tanganyika;

(j) Watu wawili walio na mafunzo na uzoefu wa usimamizi wa haki za makosa ya kijinai, ambao mmoja kati yao atakuwa na uzoefu wa kiutendaji katika elimu ya jinai na adhabu za sheria na uendeshaji wa jela; na

(k) Mratibu wa Kitaifa wa Huduma za Jamii;

(3) Kamati ya Kitaifa inaweza, wakati wowote kushirikiana na watu wasiozidi watatu ambao usaidizi au ushauri ambao itauhitaji au itaona ni muhimu katika utekelezaji wa kazi zake kwa kipindi itakachoona kinafaa.

(4) Kamati ya Kitaifa italazimika kuchagua, kati ya wajumbe wake, Makamu Mwenyekiti ambaye atafanya kazi kwa kipindi cha mwaka mmoja na anaweza kuchaguliwa tena.

(5) Muda wa kushika cheo kwenye Kamati ya Kitaifa itakuwa ni miaka mitatu, ingawa wajumbe wake wanaruhusiwa kuchaguliwa tena ili kutumikia kipindi kingine isipokuwa hawataruhusiwa kutumikia vipindi zaidi ya viwili mfululizo.

(6) Utendaji na usimamizi wa shughuli za Kamati ya Kitaifa utakuwa kama ilivyoainishwa ndani ya sheria hii, hata hivyo Kamati itasimamia taratibu zake.

Wajibu wa Kamati ya Kitaifa

**8.** (1) Kazi za Kamati ya Kitaifa zitakuwa:-

(a) kwa jumla ni kumshauri Waziri dhidi ya utekelezaji yakinifu wa vifungu vya sheria hii;

(b) kuratibu, kuelekeza na kusimamia kazi za maafisa huduma za jamii;

(c) kukusanya na kulinganisha habari za utendaji wa sheria hii kwa lengo la kuboresha sera ya kitaifa dhidi ya amri za huduma kwa jamii.

Sheria Na.9 ya 1985

(2) Bila kuathiri maelezo yaliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1), kupitia Mwenyekiti kushauri juu/kuhusu Kamati ya Kitaifa inaweza, hitaji lolote la ongezeko la matumizi ya vifungu vinavyohusiana na mapitio chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kwa zinazofaa ya mwaka 1985*, ili mahakama iweze kutoa amri ya huduma za jamii inayofaa kulingana na muktatha wa shauri husika.

Kamati ya Utendaji

**9.** (1) Kutakuwa na kamati ya utendaji ya Kamati ya Kitaifa ambayo itakuwa na:-

(a) mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) makamu –Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa;

(c) kamishna Mkuu wa Magereza;

(d) kamishna wa Ustawi wa Jamii;

(e) mratibu wa Kitaifa aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 10 ambaye atakuwa Katibu; na

(f) mjumbe mwingine mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya Kitaifa.

(2) Kwa mujibu wa maelekezo yoyote yatakayotolewa na Kamati ya Kitaifa, majukumu ya kamati ya utendaji yatakuwa kama yalivyoainishwa kwenye jedwali la kwanza.

Mratibu wa Kitaifa

**10.** (1) Kutakuwa na Mratibu wa Kitaifa wa Huduma kwa Jamii (na kwa mujibu wa sheria hii atatambulika kama “Mratibu wa Kitaifa”) ambaye atateuliwa na Waziri kwa kipindi cha miaka mitatu, ingawa ataruhusiwa kuteuliwa tena.

(2) Ili kuepuka mashaka, ni watu wale tu waliothibitika kuwa na elimu na uzoefu kwenye usimamizi wa haki dhidi ya makosa ya jinai na marekebisho mengine watafaa kwa uteuzi wa nafasi ya Mratibu wa Kitaifa.

(3) Mratibu wa Kitaifa pia atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Huduma kwa Jamii na Katibu kwenye Kamati ya Kitaifa na kwa mujibu wa maelekezo maalumu yatakayotolewa na Kamati ya Kitaifa au Kamati ya Utendaji, atawajibika kutunza daftari lenye kumbukumbu za amri za Huduma kwa Jamii.

(4) Kamati ya Kitaifa inaweza ikakasimu baadhi ya majukumu yake yaliyoainishwa ndani ya sheria hii kwa Mratibu wa Kitaifa kadri itakavyolazimu ili kumuwezesha kuendesha au kutekeleza majukumu ya kila siku ya Kamati ya Kitaifa.

(5) Ikiwa Mratibu wa Kitaifa hayupo au hajiwezi kwa sababu yoyote ile, Waziri atamteua mtu ili kushika nafasi hiyo kwa kipindi ambacho hayupo au hajiwezi, ingawa mtu atakayeteuliwa hataruhusiwa kushika madaraka hayo kwa kipindi kitakachozidi miezi sita, isipokuwa tu kifungu kidogo hiki hakitamzuia Waziri kuteua Maratibu wa Kitaifa mwingine ili kuziba nafasi.

Kamati ya Amri za Huduma za Jamii ya Kimkoa, Kiwilaya, Kikataa na Kijiji.

**11.** Waziri baada ya kushauriana na Kamati ya Kitaifa, kwa amri itakayochapishwa kwenye *gazeti la kiserikali*, ataanzisha Kamati za Amri za Huduma kwa Jamii katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji ambazo zitakuwa na wajumbe ili kutekeleza majukumu yaliyoainishwa kwenye amri.

Maafisa Huduma kwa Jamii.

Sura ya 247

**12.** (1) Maafisa wa Majaribio walioteuliwa chini ya Sheria ya Majaribio ya Wahalifu* watakuwa ni maafisa huduma za jamii kwa mujibu wa sheria hii.

(2) Waziri anaweza, kwa kushauriana na Kamati ya Kitaifa, kuteua maafisa huduma kwa jamii wa ziada kadri itakavyolazimu kwa mujibu wa sheria hii.

(3) Afisa huduma kwa jamii atatekeleza majukumu kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la pili.

(4) Afisa huduma kwa jamii ambaye si Afisa wa Umma, kwa mujibu wa sheria hii atalipwa kwa huduma atakazotoa baada ya Waziri kushauriana na Kamati ya Kitaifa na Waziri wa wakati huo mwenye dhamana ya utumishi wa umma, ataamua.

Maafisa Waangalizi.

**13.** Kwa madhumuni ya usimamizi wa wahalifu kwa mujibu wa sheria hii mahakama italazimika, baada ya kushauriana na Kamati ya Amri za Huduma kwa Jamii kuteua maafisa waangalizi, na afisa mwangalizi anaweza kuteuliwa kwa ajili ya wahalifu kadhaa.

Kanuni

**14.** (1) Waziri baada ya kushauriana na Kamati ya Kitaifa, anaweza akaandaa kanuni kwaajili ya kutekeleza malengo ya sheria hii ya kiujumla na yale ya kipekee bila ya kuathiri ujumla wa mamlaka kama yalivyobainishwa, kanuni hizo zitaainisha:-

(a) utaratibu wa wahalifu kutumika kwenye huduma kwa jamii na kuainisha adhabu pale kunapokuwa na uvunjifu wa taratibu hizo;

(b) utaratibu wa usimamizi na uangalizi wa wahalifu wanapotumika kwenye huduma za jamii;

(c) uhalali na wajibu wa wahalifu ndani ya jamii kwenye huduma kwa jamii;

(d) swali au masuala yanayohusiana na uteuzi wa mtu yeyote kwa ajili ya usimamizi wa wahalifu;

(e) jambo lingine lolote au kitu kinachohusiana na uendelezaji wa vifungu au madhumuni ya sheria hii.

Wajibu wa wajumbe wa Kamati ya Amri za Huduma za Jamii na maafisa Wengine.

**15.** Isipokuwa wale tu walioanishwa na sheria nyingine yoyote, hakuna kitu au tendo kitakachofanyika au kitafanyika na mjumbe yeyote wa Kamati ya Amri za Huduma za Jamii au mtu mwingine yeyote aliye na dhamana ya kutekeleza majukumu yaliyoainishwa ndani ya sheria hii, litapelekea mjumbe huyo au mtu yeyote kuwajibishwa kwa tendo hilo au kosa la kutotenda.

Makosa

**16.** Mtu yeyote atakayeingilia kwa makusudi mfumo wa usimamizi wa huduma kwa jamii au ambaye atakiuka vifungu vilivyoainishwa ndani ya sheria hii atakuwa amefanya kosa na baada ya kutiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi kiasi cha shilingi laki tano au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote faini na kifungo.

## JEDWALI LA KWANZA

## KAMATI YA UTENDAJI

**(Kifungu cha 9(2))**

Majukumu

**1.** Kamati ya Utendaji itawajibika:-

(a) katika uangalizi wa utendaji wa sekretarieti wa kila siku;

(b) katika ukusanyaji, utunzaji na uenezaji wa habari zinazohusiana na utekelezaji wa amri za huduma kwa jamii;

(c) kupeleka na kushauri Kamati za Amri za Huduma kwa Jamii juu/kuhusu sera zilizoandaliwa na Kamati ya Kitaifa;

(d) kufanya shughuli za kielimu zenye lengo la kuelimisha wananchi/jamii wajumbe na taasisi zinazoshugulika na haki za makosa ya kijinai kuhusu wajibu na madhumuni ya amri za huduma kwa jamii;

(e) kuratibiana na taasisi zingine kwenye mambo yanayohusiana, na yaliyo na faida kwenye huduma kwa jamii; na

(f) wajibu mwingine wowote itakaopewa na Kamati ya Kitaifa mara kwa mara

Vikao

**2.** (a) Kamati itakuwa na mamlaka ya kuamua na kusimamia mienendo yake na akidi za vikao vyake;

(b) Kwa mujibu wa matakwa yoyote kuhusiana na ya akidi, kamati inaweza ikatenda bila ya kujali nafasi yoyote iliyowazi ya wajumbe wake;

(c) Kamati itakutana angalau mara nne kwa mwaka;

(d) Kamati kwa busara yake inaweza kumualika mtu yeyote ambaye siyo mjumbe kuhudhuria kikao chochote, ingawa mtu huyo hatashiriki kwenye maamuzi.

## JEDWALI LA PILI

**(Kifungu cha 12(3))**

## WAJIBU WA MAAFISA HUDUMA KWA JAMII

Maafisa huduma kwa jamii watatekeleza wajibu ufuatao:-

(a) kuainisha sehemu zinazofaa za kazi;

(b) kusimamia kazi na maendeleo ya wahalifu;

(c) kuhakikisha kuwa amri za huduma za jamii zinatekelezwa na zinafanyika kwa uyakinifu;

(d) kuomba mahakamani mapitio ya amri;

(e) kusaidia au kuhamasisha upatanisho kati ya wahalifu na jamii;

(f) kuhakikisha kuwa hali ya usalama inaridhisha kwa jamii na wahalifu wanaotumikia amri ya huduma za jamii;

(g) ulinzi dhidi ya ubaguzi wa kiutendaji wakati wa kushugulika na wahalifu;

(h) kutunza taarifa za siri zinazohusiana na wahalifu;

(i) kutoa ushauri kwa wahalifu ili kuwarejesha upya na kuwaunganisha na mtu mwingine yeyote au asasi za watu zinazoshugulika na matatizo yanayofanana na hayo;

(j) kutunza kumbukumbu za sasa za utendaji wa mhalifu na tathmini yake;

(k) kuwasilisha taarifa maalum za kila kipindi zilizosawia au zihusika na Kamati ya Amri za Huduma za Jamii na za Mratibu dhidi ya wahalifu;

(l) kutoa taarifa maalumu mahakamani kabla ya hukumu;

(m) kuratibu shughuli za amri za huduma za jamii.